JAMHURI YA MUUNGANO
WA TANZANIA

# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

TOLEO LA 49
**NA. 00000394**






# JARIDA LA **NOVEMBA 2025** HADI **JANUARI 2026**

Rais Dkt. Samia asisitiza kila Mtanzania kupanda miti



# Rais Dkt. Samia asisitiza kila Mtanzania kupanda miti

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema ni jukumu la kila Mtanzania kupanda miti ili kurejesha uoto wa sili uliopotea kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Amesema hayo Januari 27, 2026 wakati akiongoza upandaji miti katika maeneo ya Bungi Kilimo na Kizimkazi, Zanzibar kama sehemu ya maadhimisho ya siku yake ya kuzaliwa na utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji miti ijulikanayo kama '27 ya Kijani'.

Dkt. Samia alisema ameichagua siku yake ya kuzaliwa kupanda miti kama ishara ya shukrani kwa Mungu na kutimiza wajibu wake wa kulinda mazingira na kuacha urithi kwa vizazi vijavyo.

Aliongeza kuwa Tanzania inakaribia kuwa na watu milioni 70, idadi ambayo itaisogeza nchi kufikia ulinzi na mustakabali endelevu wa mazingira kitaifa, ikiwa katika Watanzania milioni 30 kila mmoja atapanda na kutunza angalau mti mmoja kila mwaka.

Pia, Rais Dkt. Samia alieleza kuwa mabadiliko ya tabianchi ni uhalisia unaoathiri maisha ya wananchi kupitia ukame, mvua zisizotabirika, mafuriko, ongezeko la joto na kuongezeka kwa kina cha bahari.

Alisema upandaji na utunzaji wa miti ni miongoni mwa njia mahsusi za kukabiliana na athari hizo kwa kuhifadhi vyanzo vya maji, kuimarisha uzalishaji wa chakula, kuboresha afya ya binadamu na kulinda bioanuwai.

Hivyo, alisema kuwa ni muhimu kuhusisha watoto katika juhudi za utunzaji wa mazingira akisisitiza kuwa malezi ya mapema hujenga kizazi chenye uelewa na uwajibikaji wa kulinda maliasili za taifa.



# Makamu wa Rais awahimiza watumishi wa ofisi yake kulinda Muungano, Mazingira



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi amewasihi watumishi wa ofisi hiyo kufanya kazi kwa weledi kwa kuzingatia dhamana kubwa waliyopewa ya kusimamia suala la Muungano na Mazingira.

Dkt. Nchimbi amesema hayo wakati akizungumza na watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais katika kikao kazi kilichofanyika jijini Dodoma Desemba 05, 2025 ambapo amewataka kutambua na kuchukulia kwa uzito suala la uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwani linabeba mustakabali wa vizazi vya sasa na baadaye.

Aidha, aliwataka kujiwekea utaratibu wa kujipimia

malengo yaliyowekwa katika ofisi hiyo ikiwamo upandaji wa miti ili kuhakikisha utekelezaji wa mipango na malengo ya uhifadhi mazingira yanakuwa na matokeo mazuri na yenye manufaa.

Alisema lazima kutambua umuhimu wa suala la Muungano kwa kuhakikisha elimu inatolewa vya kutosha kwa wananchi hususani vijana kwa kuhusianisha maendeleo na mafanikio ya taifa yanategemea uimara wa Muungano.

Aliongeza kuwa kutokana na idadi kubwa ya wananchi kuzaliwa baada ya Muungano mwaka 1964, ni vema kutoa elimu ya kuwafahamisha umuhimu na manufaa ya Muungano ili kuendeleza mafanikio mazuri yaliyopatikana katika serikali zilizopita.

Halikadhalika, Makamu wa Rais alisisitiza umuhimu wa ofisi kujipanga kuhakikisha inatekeleza maazimio na mipango ya kulinda mazingira iliyofikiwa katika mikutano ya kimataifa ambayo Tanzania inashiriki.

Balozi Dkt. Nchimbi aliwataka pia watumishi hao kuzingatia ahadi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alizotoa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu na kuyatekeleza kwa ufanisi.

Pia aliwasihi watumishi wa ofisi hiyo kuisoma na kuelewa vema Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ili kubaini maeneo ambayo Ofisi ya Makamu wa Rais inahusika na kuhakikisha yanatekelezwa.



# DKT. NCHIMBI: Mapinduzi ya Zanzibar yameboresha sekta ya elimu



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshmiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi amesema maendeleo yanayoonekana katika sekta mbalimbali Zanzibar ikiwamo ya elimu, ndiyo lilikuwa lengo la Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Dkt. Nchimbi amesema hayo Januari 09, 2026 wakati wa ufunguzi wa Skuli ya Sekondari ya Makunduchi iliyopo Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar ikiwa ni shamrashamra za maadhimisho ya Miaka 62 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Amesema hivi sasa inashuhudiwa ndoto ya waasisi wa Mapinduzi Matukufu ikiendelea kutimizwa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia maendeleo ya sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Alisema fursa za masomo kwa wananchi wa Zanzibar zimeongeza ambapo wakati wa Mapinduzi mwaka 1964, kulikuwa na skuli 68 na hivi sasa kuna zaidi ya skuli 1,200.

Ameongeza kuwa sambamba na ongezeko la skuli, pia wanafunzi waliokuwa masomoni mwaka 1964 walikuwa 25,000 wakati hivi sasa zaidi ya wanafunzi 600,000 wanapata elimu pamoja na ongezeko la vyuo vikuu vitano (05) vilivyopo sasa ikilinganishwa na mwaka 1964 ambapo hakukuwa na chuo kikuu.

Halikadhalika, Makamu wa Rais alisema serikali imeendelea kufanya mabadiliko makubwa ya mitaala ambayo imejielekeza katika kufundisha katika kufikiri, kutafiti na kubuni pamoja na mafunzo kwa vitendo.

Aliongeza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeimarisha mitaala yake na kujielekeza katika ufundishaji wa kiteknolojia na kuboresha miundombinu ya maabara na madarasa na mfumo utakaowezesha vijana kujitegemea kupitia uwepo wa mkondo wa masomo ya jumla na masomo ya amali.

Alisema katika kipindi cha miaka 62 tangu Mapinduzi Matukufu, matunda ya Muungano yameonekana wazi ambapo Tanzania imeendelea kuulinda na kuutetea uhuru, umoja, maendeleo, pamoja na amani.

Makamu wa Rais amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa maendeleo makubwa katika kipindi cha miaka mitano pamoja na kulinda Muungano na amani.





# Makamu wa Rais akagua ukarabati jengo la Ofisi yake Dar-es Salaam

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi Januari 29, 2026 ametembelea na kukagua ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais iliyopo Mtaa wa Luthuli, Posta jijini Dar es Salaam.

Makamu wa Rais alikagua maendeleo ya ukarabati wa jengo la ofisi hiyo pamoja na usimikaji wa vifaa na samani katika ofisi mbalimbali zilizopo katika jengo hilo.

Dkt. Nchimbi wakati wa ziara ya ukaguzi wa jengo hilo aliambatana na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Dkt. Richard Muyungi ambapo alielezwa maboresho yaliyofanyika katika jengo hilo ambayo yanalenga kuongeza ufanisi na utendaji kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande wake, Dkt. Nchimbi aliridhishwa na hatua iliyofikiwa katika ukarabati wa jengo hilo na kuipongeza kamati inayosimamia ukarabati wa jengo hilo kwa kazi kubwa iliyofanya ya kuhakikisha jengo hilo linakamilika kwa wakati na kuanza kutumika.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Dkt. Richard Muyungi alimuhakikishia Makamu wa Rais kwamba ukarabati huo umekamilika kwa asilimia mia moja (100) na jengo kwa ajili ya kuanza kutumika Februari 04, 2026.








# Serikali yahakikisha sekta ya uchukuzi inaimarika

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi amesema serikali imejizatiti kuhakikisha sekta ya uchukuzi inaimarika ili kuliweka taifa kwenye nafasi nzuri ya ushindani wa kibiashara.

Hatua hiyo inaelezwa itawezesha kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni na kukuza mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa.

Amesema hayo Januri 16, 2026 wakati wa uzinduzi wa Jengo la Viongozi Mashuhuri katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, akisisitiza kuwa serikali imejipanga kuendelea kutekeleza miradi ya kisekta kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050, Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Taifa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2025 - 2030).

Dkt. Nchimbi alisema serikali itaendelea kuboresha miundombinu na huduma mbalimbali katika viwanja vya ndege, huduma za usafiri wa barabara, usafiri majini na usafiri kwa njia ya reli.

Alisema serikali itaendelea na uboreshaji wa huduma za Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kwa lengo kuboresha usafiri wa ndani, kuunganisha Tanzania na nchi nyingine, kupunguza gharama za usafirishaji na kuimarisha uchumi wa Tanzania na biashara za kimataifa.

Vilevile, Makamu wa Rais alisema ili kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji, serikali imedhamiria kuunganisha huduma za sekta ya uchukuzi kama vile uunganishaji wa huduma za viwanja vya ndege, usafiri wa barabara, maji na reli.

Mathalan, mradi wa kimkakati unaoendelea wa ujenzi wa barabara za Mwendokasi (BRT) kati ya eneo la Posta na Gongo la Mboto utaunganishwa na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere ili kurahisisha huduma za usafiri katika Jiji la Dar es Salaam.

Alieleza kuwa, hatua za utekelezaji zinaendelea ili kuhakikisha huduma za reli zinaunganishwa na viwanja vya ndege vya kimataifa hususan Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro.

Aidha, Makamu wa Rais alisema Jitihada hizo kubwa zinazofanywa na serikali zinalenga kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji ili kuchochea ukuaji wa uchumi kitaifa na kikanda.






# Mkutano wa AU, EU wahitimishwa kwa vipaumbele

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi ameshiriki Mkutano wa Saba wa Viongozi wa Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa Ulaya (AU-EU Summit) uliofanyika jijini Luanda nchini Angola Novemba 25, 2025.

Mkutano huo wa siku mbili, pamoja na mambo mengine umehitimishwa kwa dhamira ya kuunda mustakabali mwema na endelevu wa Afrika na Ulaya, ushirikiano mpya na imara juu ya Amani, Usalama na Utawala katika kukabiliana na vita na migogoro kote ulimwenguni.

Masuala mengine yaliyopewa kipaumbele katika mkutano huo ni pamoja na ahadi madhubuti ya ushirikiano wa kimataifa pamoja na ushirikiano imara na wa kuheshimiana katika masuala ya uhamaji.

Mkutano huo pia umedhamiria kuendelea kusaidia nchi zote za Kiafrika katika maendeleo, viwanda, kuongeza mauzo ya nje, na kuunganisha katika masoko ya kikanda, kuongeza kasi ya utekelezaji wa Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA).

Aidha masuala mengine ya kipaumbele ni pamoja na kukuza maendeleo endelevu kwa kuzingatia minyororo ya thamani kwa kuongeza uwezo wa viwanda vya ndani kushiriki katika masoko ya kikanda na kimataifa, ikiwemo uongezaji thamani wa madini adimu.

Ili kuwezesha biashara, Mkutano huo, umesisitiza umuhimu wa kudumisha uwazi, na njia zinazojumuisha mazungumzo, ikijumuisha biashara na shughuli za kimazingira, na kukuza ushirikiano kupitia kujenga uwezo na usaidizi wa kiufundi ili kusaidia nchi za Kiafrika.

Mkutano huo umedhamiria kushughulikia mabadiliko ya tabianchi na kukuza uendelevu wa mazingira, kwa kutatua changamoto pamoja zinazoletwa kwa wauzaji bidhaa kutoka Afrika kwa njia endelevu.

Mkutano huo umefanyika chini ya kaulimbiu isemayo "Kukuza amani na ushirikiano kupitia Ustawi wa Kimataifa wenye Tija" (promoting peace and prosperity through effective Multilateralism)

Katika Mkutano huo, Makamu wa Rais aliambatana na Waziri wa Kazi na Uwekezaji Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Sharif Sharif, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe.Dkt. Ngwaru Maghembe, Balozi wa Tanzania nchini Ethiopia na Mwakilishi wa Kudumu katika Umoja wa Afrika Mhe. Balozi Innocent Shiyo, Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji na Umoja wa Ulaya Mhe. Balozi Jestas Nyamanga, pamoja na wataalamu mbalimbali.

# Masauni awasihi wanahabari kulinda Muungano



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni amesema waandishi wa habari wana wajibu wa kusimamia uwepo wa taarifa zinazojenga Muungano na kuondoa upotoshaji unaoweza kusababisha mgawanyiko.

Mhe. Masauni amesema vyombo vya habari vina umuhimu wa kuhakikisha taarifa zinazochapishwa ni sahihi, zenye vyanzo vya kuaminika, kuandaa mijadala yenye tija, kuangazia mafanikio ya Muungano badala ya kusubiri changamoto.

Ameyasema hayo Desemba 23, 2025 wakati akifungua semina ya wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, na kuwataka kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya kikatiba, historia, na faida za Muungano pamoja na kutoa jukwaa la uwiano linalosikiliza sauti zote bila kujenga uadui.

“Wahariri wa vyombo vya habari wana wajibu wa kufuatilia kwa makini mada zitakazotolewa na wabobezi wetu wa masuala ya Muungano ili zitujengee weledi katika uandishi wa taarifa zinazohusu Muungano kwa maslahi mapana ya taifa letu na mustakabali wa Muungano wetu adimu na adhimu,” amesema Mheshimiwa Masauni.





Amesema Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa programu maalumu zitakazokuwa vivutio kwa vijana ikiwamo michezo na sanaa ili kuwawezesha kujifunza historia ya nchi yao.

Aidha, amesema ofisi hiyo imeandaa utaratibu wa kuhakikisha wanafunzi wanatembelea maeneo ya kihistoria sambamba na kuanzishwa kwa chaneli mahususi itakayozungumzia masuala ya Muungano pekee.

Aliongeza kuwa ukosefu wa uelewa kuhusu masuala ya Muungano miongoni mwa vijana ni changamoto inayopaswa kutatuliwa ili kuwawezesha kuenzi misingi ya nchi bila kuyumbishwa na mabadiliko ya teknolojia au upotoshaji mitandaoni.




# Mhandisi Masauni: Tanzania imepiga hatua katika michezo

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni amesema Maendeleo ya michezo yamechangiwa na juhudi kubwa za viongozi wakuu wa nchi Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambao wameweka vipaumbele katika sekta hiyo.

Amezungumza hayo Januari 24, 2026 wakati akifunga Mashidano ya mpira wa Pete ya Kombe la Muungano Zanzibar ambapo timu ya KVZ imeibuka bingwa baada ya kushinda michezo yote 10.

"Kupitia mpango wa "Goli la Mama", tumeshuhudia ongezeko la Bajeti, ujenzi wa viwanja vipya na mazingira bora kwa wanamichezo wetu, matokeo ya jitihada hizi ni wazi na tumeshuhudia Timu ya Taifa ya mpira wa miguu 'Taifa stars' imefika hadi hatua ya 16 bora ya michuano ya AFCON pale Morocco na ni kwa mara ya kwanza tangu kuanza kushiriki mashindano hayo," amesema Mhe. Masauni.

Amesema ujenzi pamoja na uboreshaji wa Viwanja vya michezo vimewezesha mashindano mbalimbali kufanyika yakiwemo mashindano ya CHAN yaliyohusisha nchi za Kenya, Uganda na Tanzania. Huu ni ushahidi kuwa Tanzania, kupitia Muungano wake, inainuka kisoka Afrika na Duniani.

Ameeleza Maendeleo haya yamewekewa chachu ya ushirikiano kati ya serikali zetu mbili chini ya wizara husika za michezo na taasisi zetu za ZFF, TFF, CHANEZA NA CHANETA ambazo zinasimamia michezo hii ya mpira wa miguu na Pete kwa weledi mkubwa sana.

"Nawapongeza viongozi wa wizara hizi na wasaidizi wao pamoja na viongozi wa ZFF, TFF, CHANEZA NA CHANETA kwa kuhakikisha wanasimamia maendeleo ya michezo nchini," ameongeza Masauni.





Aidha katika hatua ingine Waziri Masauni amewashukuru waandaji wa Mashindano haya CHANEZA na CHANETA na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kutekeleza agizo la Rais la kuimarisha Muungano kupitia michezo alilolitoa Aprili 13, 2024 wakati akipokea taarifa ya Kamati Maalum iliyowasilisha maandalizi ya Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CHANEZA Bi. Nasra Juma ameishukuru Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushiriki na kudhamini mashindano hayo ambayo yamekuwa ya ushindani mkubwa.

Amesema mashindano hayo ni muhimu kwa kuwa yamekuwa yakitoa wawakilishi wa Tanzania katika mashindano makubwa kwa Bara la Afrika na jumuiya ya Afrika Mashariki. Mashindano haya yalishirikisha timu 11, tano kutoka Zanzibar na sita kutoka Tanzania Bara.

# Dkt. Dugange aitaka NEMC kudhibiti uzalishaji kelele



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange amelielekeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuchukua hatua dhidi ya wanaozalisha kelele na mitetemo katika maeneo mbalimbali nchini.

Ametoa maelekezo hayo wakati wa kikao na bodi, menejimenti na watumishi wa NEMC wakati wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa shughuli na majukumu mbalimbali yanayofanywa na taasisi zilizo chini ya ofisi hiyo jijini Dar es Salaam Novemba 28, 2025.

Mheshimiwa Dkt. Dugange alisema sheria zinazodhibiti kelele na mitetemo zipo hivyo NEMC haina budi kuchukua hatua stahiki za kudhibiti hali hiyo ili kuwanusuru wananchi na changamoto hiyo ambayo huwaletea madhara ya kiafya.

Alibainisha kuwa yapo madhara makubwa yanayotokana na kelele ikiwamo maradhi ya saratani, shinikizo la damu na kisukari ambayo endapo hatua zisipochukukuliwa wananchi wataendelea kuathrika.

Pia alisema pamoja na kuwasaidia wajasiriamali kujipatia kipato, baadhi ya matangazo holela ya biashara ndogondogo mitaani kwa kutumia vipaza sauti bila mpangilio yamekuwa chanzo cha uchafuzi wa mazingira hivyo yanapaswa kuwekewa utaratibu mzuri.

"NEMC tuchuke hatua kwa kuwa sheria, kanuni na miongozo inayoelezea namna ya kuzuia uchafuzi wa mazingira hasa kelele ipo, leo hii ukipita mtaani nyumba 100 au 200 asilimia 20 zina kelele na mitetemo na muziki, nawaagiza mkae na TAMISEMI mje na mkakati wa kutatua changamoto hii," alisisitiza.

Kwa upande mwingine, amewapongeza watumishi wa baraza hilo kwa kazi nzuri ya kusimamia mazingira ambayo ni sekta pana na yenye mambo mengi yanayomzunguka mwanadamu.

Hivyo, aliwataka watumishi hao kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kuleta matokeo chanya kwani karibu wizara zote zinategemea usimamizi wa mazingira uliopo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.






# Ofisi ya Makamu wa Rais kuimarisha usimamizi wa mazingira kukabili mafuriko

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imesema itaendelea kuimarisha usimamizi wa hifadhi ya mazingira ili kuwaondolea wakazi wa Kilosa na maeneo mengine adha ya mafuriko ya mara kwa mara.

Hayo yamesemwa Januari 02, 2026 na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange wakati alipopewa nafasi na Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt Mwigulu Nchemba awasalimie wakazi wa Tindiga wilayani Kilosa mkoani Morogoro baada ya kukagua athari za mafuriko kutokana na mvua zilizonyesha katika eneo hilo.

Dkt. Dugange alieleza kuwa tayari serikali ngazi ya taifa, mkoa na wilaya imeshaanza utekelezaji wa mpango wa utunzaji wa mazingira kwa kusimamia upandaji wa miti katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, Naibu Waziri huyo aliwahimiza wananchi kuongeza kasi ya upandaji wa miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha kutokea kwa mafuriko ya mara kwa mara.

Alisema kuwa ni wakati sasa kila mwananchi achukue jukumu la kupanda miti angalau mitano kwa mwaka na kuitunza, hatua itakayosaidia kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Naibu Waziri Dkt. Dugange alielezea umuhimu wa upandaji miti na kubainisha kuwa maeneo yanapokosa miti ya kutosha, mvua inaponyesha husababisha mafuriko.

"Ukweli ni kwamba bado kasi ya upandaji wa miti inahitajika, mafuriko haya ndugu zangu Wana-Tindiga yanatokana na mito yetu kuwa na kina kifupi, mvua zikinyesha maji yanatapika yanakuja kwenye makazi ya wananchi na kuleta madhara makubwa," alisema.

Katika salamu hizo, Mheshimiwa Dkt. Dugange aliungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa salamu za npole kwa wananchi wa Tindiga na Wilaya ya Kilosa kwa ujumla kutokana na madhara ya mafuriko yaliyotokea.





# **Dkt. Muyungi** ataka NCMC kuyafikia masoko ya kimataifa

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Dkt. Richard Muyungi amekitaka Kituo cha Taifa cha Kufuatilia Kaboni (NCMC) kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika masoko ya kimataifa ya kaboni kwa kuimarisha miradi ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

Hayo ameyasema Januari 21, 2026 wakati wa makabidhiano ya kituo hicho kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kwenda Ofisi ya Makamu wa Rais, ambapo Dkt. Muyungi amefafanua kuwa kituo kitachangia kukua kwa uchumi wa taifa na kujenga uwezo wa Tanzania kushiriki katika biashara hiyo.

“Katika Dira ya 2050 tumejiwekea malengo ya kukusanya mapato ya dola bilioni moja kwa mwaka kutoka katika biashara ya kaboni ya nchi kavu na dola bilioni moja kutoka uchumi wa buluu” amesema Dkt. Muyungi.

Kwa upande wake, Naibu Makamu Mkuu wa SUA, Profesa Raphael Chigunda amemhakikishia Dkt. Muyungi kuwa chuo hicho kitaendelea kutoa ushirikiano wa kitaalamu katika masuala ya biashara ya kaboni ili kituo kiendelee kuibua na kuandaa miradi ya kaboni na hatimaye taifa na wananchi wanufaike.

Awali akizungumza katika hafla hiyo aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa NCMC, Profesa Eliakimu Zahabu amesema ataendelea kutoa ushirikiano kwa wataalamu wa kituo hususan katika kutafuta fursa za uwekezaji katika biashara ya kaboni.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa kituo hicho, Bi. Kathryn Kigaraba amebainisha kuwa kituo hicho kitaendelea na usimamizi wa gesijoto na biashara ya kaboni na masoko ya kaboni ili kuwa taaasisi muhimu katika mfumo wa kitaifa wa mabadiliko ya tabianchi na masoko ya kaboni.

Kituo hicho kimeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 (Marekebisho ya 2025). Kituo hicho ni taasisi ya kimkakati ya kitaifa yenye jukumu la kuratibu shughuli zinazohusiana na usimamizi wa gesijoto pamoja na biashara ya kaboni na masoko ya kaboni.



# Mpango wa Matumizi ya Maeneo ya Maji kuimarisha uchumi wa buluu



Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imezindua Kikosi kazi cha Kuandaa Mpango Kazi wa Kitaifa na hatua za utekelezaji wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji (MSP) ili kuhakikisha uchumi wa buluu unakuwa shirikishi na kuimarika.

Kikosi hicho kimezinduliwa na Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais, Bw. Abdallah Hassan Mitawi mjini Morogoro Januari 26, 2026 na kushirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali zenye uhusiano na uchumi wa buluu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Bw. Mitawi alisema Mpango Kazi wa Kitaifa wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Maji ni nyenzo muhimu inayotegemewa katika kuwezesha utekelezaji wa masuala ya uchumi wa buluu kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira na ustawi wa jamii.

Alisema kuwa uandaaji wa mpango unaoandaliwa kwa ushirikiano wa serikali na Shirika la The Nature Conservative (TNC), ni sehemu ya jitihada za kuhakikisha serikali inafanikiwa kupanga matumizi endelevu ya maeneo ya maji.

Bw. Mitawi alisema Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu (2024) na Mkakati wake wa utekelezaji (2024 - 2034) inasisitiza kupanga matumizi ya rasilimali za maji kwa njia jumuishi na endelevu hivyo kufanikiwa kuandaliwa kwa mpango kazi huo kutasaidia katika kutekeleza majukumu ya kila kamati.

"Mpango kazi ni lazima kuhakikisha uratibu madhubuti wa kitaifa kuheshimu kila upande unaotumia bahari, unahitajika msikamano wa kitaasisi kuhakikisha manufaa ya bahari yanawafikia wananchi wote hivyo, MSP ni chombo cha kuimarisha rasilimali zetu za bahari na ukanda wa pwani," alisema Bw. Mitawi.

Aidha, Bw. Mitawi alisema uvuvi, usafirishaji kupitia bahari, utalii, nishati, utafiti wa kisayansi na uhifadhi wa bayoanuayi bila upangaji makini shughuli hizi zinaweza kuleta mgongano wa matumizi ikiwamo uharibifu wa mifumo ikolojia na upotevu wa fursa za kiuchumi.

Pamoja na hayo, Naibu Katibu Mkuu alisisitiza kuwa serikali inatambua na kushukuru Shirika la TNC kwa kuwa wadau muhimu katika kuandaa mpango kazi huo wa matumzi ya rasilimali za maji kwa maendeleo endelevu.





# Serikali yaalika wadau wa maendeleo kubuni miradi ya **mazingira**



Wadau wa Maendeleo wameombwa kuendelea kushirikiana na serikali katika kubuni na kutekeleza miradi ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira nchini. Wito huo umetolewa na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Ofisi ya Makamu wa Rais, Profesa Peter Msoffe wakati akizindua Mradi wa Kuongoa Ardhi na Kurejesha Uoto wa Asili Nchini Tanzania kwa jijini Dodoma Januari 16, 2026.

Mradi huo wenye thamani ya Shilingi bilioni 5.4, unafadhiliwa Serikali ya Ujerumani na kutekelezwa na Shirika la WWF Tanzania kwa kushirikiana na serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Mashirika ya International Union for Conservation of Nature (IUCN).

Shirika lingine ni World Resource Institute (WRI) pamoja na wadau mbalimbali na kutekelezwa katika wilaya za Kilindi na Korogwe (Tanga) na Chamwino na Mpwapwa (Dodoma) zilizoathirika na uharibifu wa mazingira.

Profesa Msoffe alisema mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa Makubaliano ya Changamoto ya Bonn yaliyofikiwa mwaka 2011 jijini Bonn nchini Ujerumani kuwa dunia inapaswa kuongoa ekari milioni 350 za misitu ifikapo mwaka 2030.




Amesema kupitia makubaliano hayo, Serikali ya Tanzania imeahidi kuongoa ekari milioni 5.2 kupitia mpango wa AFR100 ifikapo mwaka 2030.

“Sote tunafahamu kuwa uoto wa asili ni rasilimali muhimu kwa ustawi wa mazingira na maisha ya binadamu, huchangia katika uhifadhi wa vyanzo vya maji, kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, kulinda bayoanuai na pia kutoa fursa za kiuchumi kwa jamii,” amesema Profesa Msofe.

Alisema changamoto hizo zitokanazo na shughuli zisizo endelevu za kibinadamu zimeendelea kuathiri mazingira na binadamu hivyo mradi huo umekuja kwa wakati muafaka ili kuisaidia serikali kuhimili na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Aliongeza kuwa mradi huo unalenga kurejesha mifumo ikolojia kwa kuhusisha jamii kikamilifu na hivyo kutarajiwa kuwa na mazingira wezeshi ya kisera na mikakati mahsusi ya kuhakikisha jamii inashiriki katika kurejesha uoto wa asili na kuleta mabadiliko chanya.

Mradi wa Kuongoa Ardhi na Kurejesha Uoto wa Asili unatarajiwa kutekelezwa katika wilaya za Kilindi na Korogwe (Tanga), na Chamwino na Mpwapwa (Dodoma) ambapo haya ni maeneo yaliyoathirika kwa kiasi kikubwa na uharibifu wa mazingira.

# Fahamu kuhusu Uchumi wa Buluu

Uchumi wa Buluu ni matumizi endelevu ya maeneo ya bahari kwa ajili ya faida za kiuchumi na kuhamasisha jamii kutambua fursa zinazopatikana kupitia bahari na vyanzo vingine vya maji.

Tafiti zimebaini kuwa asilimia 71 ya uso wa dunia ni maji na asilimia 97 ya maji hayo ni bahari na eneo la nchi kavu ni asilimia 29 tu ya uso wa dunia.

Tafiti zinaonesha takribani asilimia 80 ya mizigo na biashara duniani husafirishwa kwa njia ya maji, na kuwa usafirishaji kwa njia ya ardhi na anga hutumika kwa asilimia 20 pekee.

Ripoti ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) linaeleza kuwa uzalishaji wa samaki ulimwenguni ulifikia jumla ya tani milioni 175 mwaka 2018 ambapo tani milioni 156 zilitumika kwa chakula (chanzo cha protini).



## Manufaa ya rasilimali muhimu kuhusu Uchumi wa Buluu kwa Tanzania Uvuvi

Mwaka 2023, Tanzania ilizalisha **tani 513,802.47** za mazao ya uvuvi zenye thamani ya **Shilingi trilioni 3.5** hivyo kuongeza ajira na kipato cha wananchi.

Zaidi ya **asilimia 85 ya mazao ya uvuvi** yanatokana na maji baridi na **asilimia 15 maji bahari**, hali inayoonesha umuhimu wa rasilimali za uchumi wa buluu katika upatikanaji wa chakula nchini. Ikumbukwe kuwa samaki ni chanzo kikuu cha protini duniani.




## Mafuta na gesi




Tanzania ina takribani futi za ujazo **trilioni 57.54** za gesi asilia, kati ya futi hizo za ujazo **trilioni 47.13**, zinapatikana katika kina cha Bahari ya Hindi, hatua inayochochea uwekezaji wa kimkakati na kuongeza fedha za kigeni.

## Usafirishaji na biashara

Tanzania ina bandari **rasmi 86** na zisizo **rasmi 885**, hali inayoonesha nafasi ya Uchumi wa Buluu katika kuimarisha sekta ya biashara na usafirishaji. Shehena ya mizigo iliyohudumiwa bandarini imeongezeka kwa **asilimia 81** kutoka **tani 13,727,770** mwaka 2012/13 hadi **tani 24,899,000 mwaka 2022/23**, hivyo kuchochea ukuaji wa biashara na uchumi kwa ujumla.



## Utalii wa baharini na pwanii



Sekta ya utalii wa majini inaendelea kukua, ambapo kwa **mwaka 2023** idadi ya meli za kitalii iliongezeka hadi kufikia meli nane zilizowaleta **watalii 965** nchini. Ukuaji huu unaongeza mapato ya taifa na kuchochea maendeleo ya jamii za pwani.

## Kuhifadhi mazingira (Mikoko)

Tanzania ina misitu ya mikoko yenye ukubwa wa kilometa za **mraba 1,440** na miamba ya matumbawe yenye ukubwa wa kilometa za **mraba 3,580**, rasilimali ambazo ni muhimu kwa uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi. Uchumi wa Buluu unalenga kuhakikisha rasilimali hizi zinatumika kwa njia endelevu ili kulinda mazingira na kuendeleza uchumi kwa wakati mmoja.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

**JARIDA HILI LIMETOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**Ofisi ya Makamu wa Rais**

Barua pepe: **ps@vpo.go.tz**

**blog.vpo.go.tz**

